Toleo 40

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## TWAONGOZWA NA MCHUNGAJI

Nitafanyaje? Je, nitaishi hapa ama niishi kwingine? Je, nitaendelea na masomo yangu? Je, nijifunze taaluma gani ya maisha? Kwa kweli huyu ndiye ninayestahili kuoa? Je, nitahudhuria kanisa gani? Je, ni jambo lipi linafaa nifanye? Mungu anataka niishi vipi, na angetaka nifanye nini maishani? Katika tukio hili ni jambo gani ambalo linafaa mimi kufanya? Mimi sijui nifanye nini katika changamoto hii ambayo imenipata. Kwa kweli nimechanganyikiwa kabisaa!

Maisha haya yetu yanaweza kujaa maswali mengi, hali ya kuchanganyikiwa, na maamuzi mengi ambayo tunastahili kufanya. Maamuzi mengine huwa mazito na yenye matokeo makubwa; mengi hata huweza kubadilisha mwelekeo wa maisha yetu yote. Habari njema ni kwamba hauna haja ya kukabiliana na changamoto hizi ukiwa peke yako, au kwa kutumia hekima yako. Mungu anajali maisha yako sana, na anao mpango kabambe kwa ajili ya maisha yako. Kwa kweli jambo la kwanza kabisa ambalo Mungu hushughulika nalo katika maisha yako ni kuendelea vizuri kwa maisha yako ya kiroho. Lakini pia Yeye hujali sana kuhusu mambo yote ambayo yanaathiri maisha yako.

Watu wengi huwa na imani na hekima yao, ufahamu wao, uongozi wa nia yao, au hisia zao; kwamba haya ni mambo ambayo yanaweza kuwaongoza kwenye maamuzi ambayo wanahitaji kufanya. Lakini kwa kweli ushahidi mwingi ambao tunapata kutokana na hatma ya maisha ya watu ambao wametuzunguka unaunga mkono andiko ambalo linapatika katika Yeremia 10:23 "Ee BWANA, najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu." Wanadamu hawakuumbwa kuishi bila mwongozo wa Muumbaji wao. Mipango na njia za mwanadamu zitamwongoza mtu kufanya maamuzi ambayo hayafai na kupata matokeo ambayo yanaweza kumletea mauti. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; lakini mwisho wake ni njia za mauti" (Mithali 16:25). Sisi tuna mwokozi na rafiki ambaye ana ufahamu wote, uelewaji wote, na pia ana nguvu na shauku la kutembea nasi katika maisha yetu yote. Wewe ukimruhusu hatakuongoza tu hadi kufika mbinguni bali pia ataweza kukuongoza na kukuonyesha njia wakati ambapo utahitaji kufanya maamuzi ambayo yana uwezo wa kubadilisha mwelekeo wa maisha yako. Mungu anajali maslahi yako, na Yeye atakuongoza ili tuweze kupitia mitego na changamoto zote za maisha haya.

Hata ingawa kuna mambo mengi ambayo hatuwezi kuwa na uhakika nayo, na ambayo yanaweza kukuletea hali ya kusumbuka na kuwa na wasiwasi, Mungu hataki tutembee katika giza au katika hali ya kuchanganyikiwa. Yeye ndiye Mchungaji Mwema ambaye anatuongoza hadi katika maji matulivu. Yeye anataka kuwa ndiye anayetutunza, rafiki yetu, na juu ya yote aweze kutembea nasi kupitia kwa bonde za mauti.

Sura ya kumi ya Injili ya Yohana inasema Yesu ndiye Mchungaji Mwema. "Bawabu humfungulia huyo, na kondoo humsikia sauti yake; naye huwaita kondoo wake kwa majina yao, na kuwapeleka nje. Naye awatoapo nje kondoo wake wote, huwatangulia; na wale kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti yake. Mgeni hawatamfuata kabisa, bali watamkimbia; kwa maana hawazijui sauti za wageni" (mstari 3-5).

Yesu anajua jina lako, na Yeye anaona maamuzi na uchaguzi ambao unahitaji kufanya kwa mambo ambayo yako mbele yako. Sauti ya Yesu itaingilia kati katika

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Mungu anajali maslahi yako, na Yeye atakuongoza ili tuweze kupitia mitego na changamoto zote za maisha haya."


Tahariri 3

Mafundisho ya Biblia: Vile Unaweza Kujua Mapenzi ya Mungu 4

Vile Unaweza Kujua Mapenzi ya Mungu 5-8

Maswali na Majibu 9

Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 10

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

hisia zako na vile unavyojisikia, na ataweza kukupatia mwongozo na faraja. Yeye ataenda mbele yako, na kuangaza njia ambayo unapitia. Swali ni – je wewe utafuata mwongozo wake? Watoto wa Mungu wanajua sauti ya Mchungaji wao na wataweza kumfuata, huku wakitoroka kutoka kwa sauti na njia zingine ambazo zinawakabili. Ni wakati watu wameanza kumsikiliza mgeni ndipo wao hujipata kwamba wanaendelea kuwa mbali sana na Kristo, mbali na utakatifu wake, na mbali na Neno lake Mungu.

Kuna nyakati ambapo utahisi kwamba Mungu kamwe hakuongozi, lakini ukiwa na subira na kumsikiliza Yeye, sauti yenye faraja ya Mchungaji itanena tena na kukuongoza katika njia za utakatifu. Hatuna haja na hatustahili kamwe kufanya njia zetu wenyewe za kufuata, kwa sababu tukifanya hivyo tutakwenda mrama maishani. Lakini tukimfuata Kristo na njia zake tutafika kwenye matarajio yetu na kuwa na amani na ushindi.

> “Mungu ametupa sisi wanadamu vipawa, vifaa vya kufanya kazi, na vitu vyote ambavyo tunahitaji ili kuweza kujua mapenzi yake (kamili) kwa ajili ya maisha yetu.”

Kama utatafuta mapenzi ya Mungu juu ya shauku na kusudi zako, muda si muda na kwa wakati unaofaa Yeye atakuonyesha kile ambacho unastahili kujua na kufanya. Katika uaminifu wake Mungu ametupa sisi wanadamu vipawa, vifaa vya kufanya kazi, na vitu vyote ambavyo tunahitaji ili kuweza kujua mapenzi yake (kamili) kwa ajili ya maisha yetu. Ni kweli kwamba hata wakati ambapo tunatafuta mapenzi yake Mungu tutafanya makosa, lakini kama vile tutaendelea kukua ndani yake Bwana, na kujifunza kutoka kwake, tutaweza kuelewa sauti yake na njia zake kwa kiwango kilicho dhahiri zaidi.

Bwana atawaongoza watoto wake. Yeye atatuongoza kwa mambo ya kiroho na kutusaidia kujua na kuishi maisha ambayo yanampendeza Baba. Katika maamuzi yetu yote makuu tunaweza kuongozwa na Mchungaji. Basi tusimzuie au kufanya maamuzi ambayo yanafuata muda tuliojiwekea sisi wenyewe, bali tumfuate Yeye kwa uangalifu na kwa ukweli.

Ni faraja kubwa mtu kupata tulizo lake ndani yake Mungu, hata katika nyakati ambapo hajui afanye nini, wakati mawazo na hisia zake zinahitilafiana. Mungu mwenyewe, kwa njia ya Neno lake, kwa njia ya Roho Mtakatifu, atatuongoza kwa hekima, kwa uelewaji bora, na kwa huruma zake. Basi hebu tutafute uongozi wake Bwana na tuweze kuongozwa na Mchungaji. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*BWANA naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku.* —Kutoka 13:21

Kama vile Bwana aliwatangulia wana wa Israeli ndani ya wingu mfano wa nguzo mchana, na ndani ya moto mfano wa nguzo usiku ili apate kuwaongoza, ndivyo atakuwa mwaminifu kuongoza watoto wake hata siku zetu. Mungu hajatuachilia tufuate mipango yetu sisi wenyewe ambayo inaweza kutupeleka Mbinguni. Yeye hajatuwacha peke yetu ili tutumie fikira na hekima yetu wenyewe kufanya maamuzi makubwa maishani mwetu ambayo yatabadilisha maisha yetu kwa njia kubwa. Mungu ameahidi kwamba atatuongoza na kuwa pamoja nasi.

Mzigo nilio nani katika robo hii ya mwaka ni kushiriki nanyi maandiko kadhaa kuhusu jinsi mtu anaweza kujua mapenzi yake Mungu. "Je, mimi naweza kujua mapenzi ya Mungu vipi?" Hili ndilo swali ambalo vijana wengi na Wakristo wengine wa umri zote huwa wanauliza. Lakini hakuna maelezo ya upishi wa jawabu hilo ambayo ukiyafuata yatakuletea jawabu sawa kila wakati. Walakini Mungu ameahidi kwamba atatuongoza, na Yeye ametupatia miongozo na njia ambazo kwa kuzifuata tutaweza kutafuta mapenzi yake. Swala la kujifunza ili kujua mapenzi yake Mungu ni jambo ambalo huchukua muda mwingi na pia ujuzi. Haijalishi sisi tumemtumikia Bwana kwa miaka mingapi, Mungu anataka tumtegemee.

*Tutembelee*

*www.thegospeltruth.org*

*ili kujiandikisha na*

*kupata jarida*

*za mbele.*

Wakati unaofaa wa Mungu ni wa kustajabisha. Kuna nyakati ambapo mimi nimemtafuta Mungu kwa miezi mingi ili aweze kunipa mwongozo wake. Halafu Bwana anazungumza, na papo hapo ukungu wa hali ya kuchanganyikiwa unaondoka. Kama vile wimbo mmoja unavyosema, "Mimi najua utamu mzuri wa sauti yake." Furaha yangu ni kwamba unaweza kujua sauti yake Mungu. Hii ni sauti ambayo iko tofauti na sauti zile zingine zote.

Katika mafunzo haya yetu tutazama kimuhstasari njia tofauti ambazo Mungu hutumia kuwasiliana nasi kuhusiana na mapenzi yake katika maisha yetu. Si jambo la busara sisi kuamini ushahidi wa mtu mmoja, kwa sababu tunaweza kujipata tumeenda mrama, lakini kwa ushahidi wa watu wawili au watatu, tunaweza kwenda mbele kwa imani na ujasiri.

Hata ingawa ninatoa onyo kuhusu sisi kutumia njia ya ngozi ya mbuzi, kwa kweli wakati mwingine Mungu anatumia njia hiyo. Kuna wakati ambako kulikuwa kunafanyika mabadiliko makubwa maishani mwangu ambapo niliamini kwamba Roho wa Mungu alikuwa anatuongoza. Nikamwomba Mungu kuhakiki jambo hilo kwa kutumia njia ya ngozi ya mbuzi—maanake kwa kutumia njia ambayo si ya kawaida. Baadaye kidogo Mungu alihakiki Neno Lake kwa uongozi wa Roho wake kwa kuhakiki njia hiyo ya ngozi ya mbuzi. Jambo hilo halikuwa limetendeka hapo mbeleni maishani mwangu, na kwa kweli kutoka wakati huo halijawahi tendeka tena. Pia kuna wakati mwingine maisha yangu yalikuwa katika hali ya hatari na nilihitaji uhakiki kutoka kwake Mungu. Na hata ingawa sauti ya Mungu haikuwa ya wazi, Yeye alinena nami kama kwamba alikuwa mahali hapo, kama kwamba tulikuwa tukizungumza ana kwa ana. Kusema kweli nyakati hizo hazikuwa za kawaida, na nimekuja kujua kwamba kwa kawaida Mungu hafanyi kazi hivyo. Lakini kwa kweli Mungu ametuongoza sisi kwa Neno na kwa Roho wake kwa miaka mingi, na mimi ninakuhakikishia kwamba wewe pia waweza kumwamini Bwana.

Ushirika wako wa kila siku na Mungu ni faraja na usalama wakati Yeye anayaongoza maisha yako. Ndiposa mimi natoa changamoto kwa kila Mkristo kwamba tumtafute Mungu ili aweze kukuongoza katika ndoa yako, fedha zako, kazi yako ya kulea watoto, ibada zako, na kwa hakika katika kila maamuzi makubwa maishani mwako. Mungu atakuwa mwaminifu kutimiza ahadi yake ya kukuongoza, mradi tu utamtafuta na kusubiri kupata uongozi wake.

Michael W. Smith

Aprili, 2022

Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.
Mithali 3:5-6



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Vile Unaweza Kujua Mapenzi ya Mungu

**Somo la Maandiko:** *Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana.* —Waefeso 5:17

**Muhstasari:** Mungu ametupatia vifaa na rasilmali ambazo kwa kuzitumia tunaweza kujua na kuelewa mapenzi yake katika maisha yetu ya kibinafsi.

### I. Umuhimu wa Kujua Mapenzi ya Mungu

A. Yeremia 10:23 Mwanadamu haelekezi hatua zake.
B. Mithali 16:25 Njia ya mwanadamu yaleta mauti.

### II. Waweza Kujua Mapenzi yake Mungu

A. Mithali 3:6 Mungu atanyosha mapito yako.
B. Waefeso 1:8-9 Kristo atatujulisha mapenzi yake.
C. Wakolosai 1:9 Kujua mapenzi ya Mungu

### III. Mapenzi ya Mungu kwa Watu Wote

A. 2 Petro 3:9 Watu wote watubu.
B. Warumi 12:1-2 Kujua mapenzi ya Mungu kwa uhakika.
C. 1 Petro 1:15-16 Kuwa watakatifu katika mwenendo wote.
D. 1 Petro 2:21-23 Kufuata nyayo za Kristo.
E. 1 Wathesalonike 4:3 Utakaso
F. 1 Wathesalonike 5:16-18 Furahini, ombeni, shukuruni.

### IV. Jinsi Mungu Hudhihirisha Mapenzi Yake

**A. Neno la Mungu**
1. Zaburi 119:105 Mwanga wa njia yetu.
2. 2 Timotheo 3:15-17 Lafaa kwa mafundisho.

**B. Roho Mtakatifu**
1. Yohana 16:13 Atawaongoza kwenye ukweli wote.
2. Warumi 8:14 Kuongozwa na Roho Mtakatifu.
3. Isaya 30:21 Masikio yako yatasikia neno.

**C. Sauti ya Mungu**
1. Mathayo 17:5 Mungu anena kutoka kwa wingu.
2. Matendo 8:26 Malaika wa Bwana amwongoza Filipu.

**D. Mungu Huwatumia Wanadamu**
1. Waefeso 4:11-13 Huduma ya Kanisa.
2. Waebrania 13:17 Kunyenyekea viongozi wa huduma yake Mugu.
3. Mithali 11:14 Umuhimu wa kupata mashauri.

**E. Matukio Katika Maisha Yetu**
1. Warumi 8:28 Mambo yote hutenda kazi kwa wema.
2. Matendo 16:6-7 Mipango ya mtume Paulo yazuiwa.

**F. Ngozi ya Mbuzi**
1. Waamuzi 6:36-40 Gideoni aweka ngozi ya mbuzi.
2. Mathayo 12:38-40 Kukemewa kwa kutaka ishara.

**G. Maono na Ndoto**
1. Matendo 2:17 Roho atapeana maono na ndoto.
2. Mathayo 2:13 Malaika amwonya Yusufu.
3. Matendo 10:9-10, 19-20 Maono ya Mtume Petro. Yahakikiwa na Roho.

### V. Vile Tunaweza Kutafuta Mapenzi ya Mungu

**A. Kutafuta kwa Shauku**
1. Mathayo 6:33 Tafuteni kwanza.
2. Zaburi 143:10 Nifundishe kufanya mapenzi yako.
3. Zaburi 25:4-5,9 Niongoze katika ukweli wako.
4. Mithali 3:5-7 Mkiri Mungu.

**B. Omba kwa Uwazi ili Kupata Imani**
1. Yakobo 1:5-6 Omba kwa imani ili upate hekima.

**C. Mkaribie Mungu**
1. Hosea 6:3 Nasi natujue.
2. Yakobo 4:8 Tumkaribie Mungu.

**D. Kusikiliza**
1. Zaburi 46:10 Kutulia.
2. Yakobo 1:19 Uwe wa haraka kusikia.

**E. Kuwa na Subira**
1. Zaburi 27:14 Kumngoja BWANA.

**F. Jisalimishe kwa Mapenzi ya Mungu**
1. Mathayo 23:37 Lakini hamkutaka.
2. Luka 22:42 Sio mapenzi yangu.

### VI. Kutii

A. Waefeso 6:6-7 Kutoka moyoni.
B. Isaya 1:19 Kukubali na kutii.

Tamati

*Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.* —1 Yohana 2:17

# Vile Unaweza Kujua Mapenzi ya Mungu



Mungu analo shauku na kusudi la kuwa na ushirika na watoto wake. Yeye ameahidi kwamba atatuongoza na kutuonyesha njia, na kupitia kwa vipawa vya kiungu, na pia vifaa vya Kiroho, sisi twaweza kujua mapenzi yake kwa ajili ya maisha yetu ya kibinafsi. Ikiwa tutafaulu kwa mambo ya kiroho hatuna budi kuwa na hekima na "kufahamu mapenzi ya Bwana" (Waefeso 5:17).

## Mungu Ataka Kudhihirisha Mapenzi Yake

"Basi mapenzi ya Mungu kwa wanadamu wote yanahitaji kuwa msingi ambao mtu kibinafsi atatumia ili kupata mwongozo wa maisha yake."

### Ahadi za Kupata Uongozi

Ahadi zake Mungu ni za hakika na zinamhusu kila mtu katika kizazi hiki ambaye anatii masharti yake. Katika Mithali 3:6 tunaambiwa kwamba, "Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako." Kama mtoto wa Mungu atamtambua Mungu na kumpatia nafasi ya kufanya kazi maishani mwake, Yeye atamwonyesha mapenzi yake na mpango wake kwa maisha yake. Mafumbo na maswali maishani haya yanaweza kujibiwa kwa sababu Kristo "Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na uradhi wake" (Waefeso 1:9). Hata ingawa ulimwengu utakejeli na kudharau Wakristo, watakatifu wa Mungu wanaweza kumtumaini na kupata kitulizo chao kutoka kwa Bwana: "Ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni" (Wakolosai 1:9). Je, ni faraja na nguvu gani tunazopata wakati tukikabiliana na changamoto na shida za maisha haya huku tukijua kwamba Mungu, kwa hekima yake isiyo na kipimo, atatuongoza kwa njia ambayo itaambatana na uwezo wetu wa kuelewa mapenzi yake. Tunaweza kufanya maamuzi makubwa maishani mwetu kwa ufahamu na nguvu zake Mungu, badala ya kutumia hekima ya kilimwengu au hisia zetu na jinsi tunavyojisikia, ambayo ni mambo yasiyo na utimamu.

### Mapenzi ya Mungu kwa Watu Wote

Mungu ana mapenzi ambayo ni ya jumla kwa wanadamu wote, lakini pia Yeye ana mapenzi na mpango kabambe kwa kila moja wetu. Mapenzi hayo ya kibinafsi kamwe hayawezi kwenda kinyume au kudhalilisha mapenzi ya Mungu kwa watu wote, kama ambavyo imeonyeshwa katika Maandiko. Basi mapenzi ya Mungu kwa wanadamu wote yanahitaji kuwa msingi ambao mtu kibinafsi atatumia ili kupata mwongozo wa maisha yake. Mungu "hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9). Kama jinsi ambavyo anataka kila mwanadamu aokolewe, pia ni mapenzi yake kwetu kwamba "Msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:1-2). Watu ambao wanaomba mapenzi na uongozi wa Mungu kufanyika maishani mwao wanapoteza wakati wao ikiwa maishani mwao hawafuati mapenzi ya Mungu kwa wanadamu wote. Mungu hana wajibu wa kujibu maswali ambayo yanamletea mtu wasiwasi na ugumu wa maisha kama mtu huyo kwanza hayuko tayari kujitoa kwa mapenzi ya Mungu ambayo tayari yamedhihirika kwa uwazi katika Maandiko.

Mungu ana mapenzi ya jumla kwa watu wote, kwamba sisi watoto wake tuwe "Watakatifu katika mwenendo wenu wote" (1 Petro 1:15). Hakuna haja ya mtu kuomba uongozi wa Mungu kwa jambo ambalo litampeleka zaidi karibu na ulimwengu au kumpeleka mbali sana na Mungu, kwa maana haya SIO mapenzi yake Mungu. Kutoka 1 Wathesalonike 4:3 tunaona ni mapenzi dhahiri ya Mungu kwamba tunahitaji kuiga mfano wake Yesu, kwa kuishi maisha ambayo hayana dhambi, matakatifu, ya kusameheana, na ya upendo (1 Petro 2:21-23). Ni mapenzi ya Mungu ambayo tayari yashaandikwa, kwamba tupate kutakaswa (kutengwa na ulimwengu ili tuweze kutumiwa na Bwana wetu peke yake). Hatuna budi kufurahi, kuomba, na kutoa shukrani kwa maana "Hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu" (1 Wathesalonike 5:16-18).

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

# Vifaa vya Kutumia ili Kuweza Kujua Mapenzi Yake Mungu

*Mungu ametupatia vifaa kadhaa na hata vipawa ambavyo kupitia kwake twaweza kujua mapenzi yake ya kiungu kwa watu wote, na hasa kwa maswali ambayo yamo maishani mwetu. Mungu ametupatia mashahidi wawili hapa duniani ambao humshuhudia Yeye na pia kushuhudia mapenzi yake—mashahidi hao ni Neno lake na Roho wake.*



"Hata wakati ambapo amenena kupitia kwa Neno lake, au kupitia kwa Roho Mtakatifu, kunakuwa mwangaza dhahiri, na sauti inayofika kwenye masikio ya kiroho ya mwanadamu kamwe haiwezi kuacha tukiwa na shaka kwamba ni Mungu anayezungumza."

## *1. Neno la Mungu*

Zaburi 119:105 inasema "Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu." Biblia ni daftari ya mwongozo wa vile ambavyo tunaweza kuishi maisha ya kitauwa. Biblia ina majibu mengi ya maswali ya kibinafsi ambayo watu huwa nayo, sio tu kuhusiana na maswala ya kiroho, bali pia kuhusu ndoa, kulea watoto, fedha, nk. Neno la Mungu ni rasilmali kuu sana ya mtu kuweza kujua mapenzi yake Mungu, lakini ni jambo ambalo huchukua muda na bidii ya mtu kuisoma Biblia kwa moyo na fikira zilizo wazi. Neno la Mungu "Lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Timotheo 3:15-17). Mungu mwenyewe anaweza kuhuisha andiko fulani ambalo ndilo linampatia mtu jibu ambalo alikuwa akitafuta. Lakini makosa yanaweza kufanyika ikiwa andiko halitatafsiriwa vilivyo, au kutumiwa katika mahali ambako halifai. Watu ambao wanataka kwenda mahali fulani wanaweza kupata andiko ambalo linawaambia "waende." Pia wanaweza kupata andiko ambalo linawaambia "wakae nyumbani." Watu wengi wenye misimamo mikali wameweza kugeuza maandiko kwa ajili ya manufaa yao wenyewe, nje ya mapenzi yake Mungu. Walakini, Mungu hutumia Neno lake, na kwa kweli Yeye anatumia Neno lake, kwa njia ya uvuvio wa Roho wake, ili kutoa miongozo timamu kwa watu ambao wanatafuta majibu kwa roho ya ukweli.

## *2. Roho Mtakatifu*

Mungu alitoa kipawa maalum cha Roho Mtakatifu kwa watoto wake. Roho Mtakatifu alikuja ili atuongoze "kwenye kweli yote" (Yohana 16:13), na watoto wa Mungu "Wanaongozwa na Roho wa Mungu" (Warumi 8:14). Lakini ni jambo ambalo huchukua muda mtu kujifunza vile ambavyo Roho Mtakatifu huwaongoza watu, jinsi Yeye huwaonyesha njia, na hata kuwapatia uvuvio. Ni jambo la ajabu unapomtafuta Mungu halafu masikioni mwako unasikia "neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni" (Isaya 30:21). Wakati Roho Mtakatifu anatuongoza Yeye hutuongoza kutoka ndani kabisa ya nafsi yetu, na sauti yake huwa tofauti na mawazo ya akilini mwetu, ambayo hutwingia na kutoka. Yeye anafanya kazi yake kupitia kwa uvuvio, na kwa sisi kujisikia mzigo mioyoni mwetu, na kama kwa kweli ni Roho Mtakatifu anayefanya kazi wakati huo, uongozi wake unakuwa dhahiri na wa wazi kabisa. Lakini kamwe Roho Mtakatifu hawezi kunena kinyume na Neno la Mungu, wao daima huambatana. Basi mtihani mkuu wa kujua mapenzi yake Mungu ni kuona kwamba Neno la Mungu na Roho wake wamepatana na kuandamana na wale mashahidi wengine wasaidizi.

## *3. Sauti ya Mungu*

Kuna nyakati ambazo Mungu amenena kwa sauti inayosikika, kama wakati aliponena kutoka kwa wingu katika Mlima wa Kugeuzwa, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye" (Mathayo 17:5). Naye malaika wa Mungu alinena na Filipo na kumwambia aende huko Gaza (Matendo 8:26).

Hata ingawa itaonekana kwamba mambo yatakuwa rahisi wakati Mungu akisema nasi kwa sauti ya moja kwa moja ambayo tunaweza kuisikia, lakini hata wakati ambapo amenena kupitia kwa Neno lake, au kupitia kwa Roho Mtakatifu, kunakuwa mwangaza dhahiri, na sauti inayofika kwenye masikio ya kiroho ya mwanadamu kamwe haiwezi kuacha tukiwa na shaka kwamba ni Mungu anayezungumza.

## *4. Mungu Huwatumia Wanadamu*

Wakati mwingi Mungu huwatumia watu wale wengine kama mashahidi wa Neno na Roho

kwa watu ambao wanatafuta uongozi wake. Hata igawa kuna sauti nyingi ulimwenguni, mhudumu wa kweli wa Injili na mshauri anayeongozwa naye atanena kile ambacho kinalingana na mashahidi wale wawili wa mstari wa mbele. Mungu ameweka kazi ya huduma Kanisani ili mwili wake uweze kukamilishwa na kutiwa nguvu (Waefeso 4:11-13). Wakati kuna maswali ambayo yanahitaji mwongozo wa Mungu, wakati mwingine Yeye huwatumia wahudumu wa Injili ili kuwahakikishia Wakristo mapenzi yake Mungu. "Pasipo mashauri taifa huanguka" (Mithali 11:14), na ni rasilmali kuu mtu kutafuta mashauri ya kiungu katika maamuzi yake makuu ambayo yanaweza kubadilisha maisha yake, hasa katika masuala ya maisha ya kiroho.

### 5. Matukio Maishani Mwetu

Matukio maishani mwetu ni njia nyingine ambayo Mungu hutumia kudhihirisha mapenzi yake. Jambo hili hutendeka hata kwenye matukio ambayo yanaonekana kuwa ya kawaida kabisa, ambapo tunapata kwamba milango fulani imefunguka au kufungwa katika maisha yetu. Kama mtu anatafuta uongozi wa Mungu katika mambo mawili ambayo yako mbele yake, halafu nafasi moja ifungike, jambo hilo hudhihirisha mapenzi ya Mungu. "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema" (Warumi 8:28). Hata ingawa Mungu hatumii matukio ya maisha yakiwa peke yake, mtoto wa Mungu anaweza kuamini kwamba Mungu ndiye ambaye anamuongoza na kutengeneza njia katika hali ambayo itawezesha mapenzi yake kufanyika katika maisha ya mtumishi wake. Mipango yetu inaweza kuzoroteshwa na hali ambazo zimetukumba, na ni jambo muhimu sisi kujifunza tofauti iliyoko kati ya kupitia hali ya ugumu wa maisha haya ambayo tunahitaji kushindana nayo, na pingamizi ambazo zinatukumba na ambazo kusudi lake ni kutuongoza ili tuwe na mwelekeo tofauti maishani mwetu.

### 6. Ngozi ya Mbuzi

Katika Agano la Kale Gidioni aliweka ngozi ya mbuzi mbele yake Bwana ili yeye aweze kujua mapenzi ya Mungu (Matendo 6:36-40). Hata ingawa kuna nyakati ambapo Mungu ametumia njia hii ya 'ngozi ya mbuzi' kuonyesha mapenzi yake, Kristo aliwakemea Wayahudi katika Mathayo 12:38-40 kwa sababu ya wao kutafuta ishara ili kuamini. Wakati ambapo ishara hiyo haijafika,



hii si kusema kwamba hayo ndiyo mapenzi ya Mungu. Lakini sio vizuri njia hii ya "ngozi za mbuzi" kutumiwa wakati mwingi, na pia inahitaji kutumiwa kwa uangalifu. Zaidi ya hayo njia hiyo ya kung'amua mapenzi yake Mungu inahitaji kutumiwa chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu wa Mungu. Sisi hatuna haki ya kumwambia Mungu njia ambayo anastahili kutumia ili kudhihirisha mapenzi yake.

### 7. Maono na Ndoto

Vivyo hivyo maono na ndoto ni njia ambazo zinahitaji kutumiwa kwa uangalifu mwingi, na pia sisitumiwe vibaya. Matendo 2:17 inasema kwamba wakati Roho Mtakatifu alipotumwa "Vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto." Katika Mathayo 2:13 Yusufu alipokea maagizo katika ndoto, ndiposa akatorokea Misri. Pia Mungu alimfundisha Petro somo kuhusu kuwakubali Mataifa kupitia kwa ndoto iliyohusiana na mtu kula wanyama wachafu (Matendo 10:9-10). Ni jambo la kuzingatia kwamba katika tukio hili Roho Mtakatifu alihakiki ndoto hiyo kwa Petro katika mstari 19-20: "Roho akamwambia . . . ondoka ushuke ufuatane nao, usione tashwishi, kwa maana ni mimi niliyewatuma." Mungu anaponena kwa njia ya ndoto na maono, daima njia hizo mbili hukubaliana na mashahidi wale wengine. Na maana ya ndoto na maono hayo itakuwa dhahiri, sio ambayo imefichika, na pia haitakuwa mchanganyiko wa mambo yasiyo na utaratibu mzuri kama inavyokuwa katika ndoto zetu za kawaida. Lakini wewe kuwa mwangalifu ili usiwe mtu wa kutafsiri Mungu katika kila ndoto unayoipata.

## Vile Tunaweza Kutafuta Mapenzi ya Mungu

*Lengo la Mungu na shauku lake ni kudhihirisha mapenzi yake, na pia kuwaongoza watu wake. Hakuna haja ya mapenzi yake kuwa fumbo katika sehemu yoyote ya maisha yetu. Lakini kwa kawaida Mungu hajibu maswali yetu kwa mwangwi wa nguvu kutoka angani. Kuna njia ambayo inafaa ya kutafuta mapenzi ya Mungu huku pia tukitumia mashahidi na vifaa ambavyo ametubariki navyo.*

### 1. Kutafuta kwa Shauku

Tunahitaji kutafuta mapenzi ya Mungu kwa shauku kubwa la kutaka kumpendeza Bwana. "Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33). Watu ambao hawamweki Mungu nambari moja katika kila fani ya maisha yao wakati mwingi hawatapokea majibu ambayo wanatamani kupata. Kunahitaji kuwa na shauku ya kujifunza, na pia roho ya kutaka kupokea. "Ee BWANA, unijulishe njia zako, unifundishe mapito yako" (Zaburi 25:4-5). Mungu atawaongoza watu wapole (Zaburi 25:9) na atamwongoza mtu ambaye anatafuta uongozi wake kwa bidii (Mithali 3:5-7). Wakati majibu yamechelewa kufika, hiyo itakuwa ni kama vile barua

*(Endelea katika Ukurasa 8)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 7)

pepe hutumwa lakini ikakosa kufika kutokana na ukweli kwamba anwani iliyotumiwa imejaa mambo yasiyofaa. Basi weka akili zako zikiwa tayari na uweze kumtatafuta Mungu kwa moyo uliojaa uwazi na ukweli.

### 2. Omba kwa Imani

"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote" (Yakobo 1:5-6). Wakati ambapo unafanya maamuzi makubwa maishani mwako na unayo haja ya uongozi wa Mungu, omba kwa ajili ya hitaji hilo, na uwe na imani kwamba Mungu atakujibu kwa wakati ambao unafaa. Unaweza kupunguza masumbufu yako ya kiakili na wasiwasi wako ukijifunza kumtumaini Mungu na kumwomba.

### 3. Mkaribie Mungu

Hosea 6:3 inatufundisha ukweli muhimu kuhusiana na swala la mtu kutaka kujua mapenzi ya Mungu: "Nasi na tujue, naam, tukaendelee kumjua BWANA." Jinsi unavyoendelea kumjua mtu ndivyo ambavyo utaendelea kujua tabia zake, mawazo yake, mambo yale ambayo anapenda, malengo yake, na hata mapenzi yake. Ni vivyo hivyo ilivyo kuhusiana na Mungu. Kulingana na jinsi ambavyo tunamkaribia Mungu ndivyo ambavyo tutazidi kuwa mbali na ulimwengu. Hivyo ndivyo tutaendelea kumjua Kristo zaidi na zaidi, na kuweza kujua Yeye ni nani, pamoja na sifa zake. Jambo hili nalo hufanya tuelewe sauti yake, na mapenzi yake kwa njia kubwa zaidi maishani mwetu.

### 4. Tulia na Usikilize

Wakati ambapo wewe umechanganyikiwa na hujui kwa uwazi mapenzi yake Mungu ni yapi, huo ndio wakati ambapo tumepewa wosia wa "Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu" (Zaburi 46:10). Huu ni wakati bora wa kutulia na kuanza kusikiza sauti nyororo ya Mungu. Mungu huyaongoza mambo yote na kamwe Yeye hatawaacha watoto wake.

### 5. Kuwa na Subira

Watoto wa Mungu wakitafuta mapenzi yake Mungu wao huweza kutambua kwamba Mungu hufanya kazi akitumia vipimo vya wakati ambavyo havilingani na vile vyetu vya kawaida. Yeye hasukumwi na wakati ule ambao tumejiwekea, na pia Yeye hasukumwi na vile ambavyo tumepanga mambo yetu. Lakini kila wakati Yeye huwa anafika kwetu kwa wakati, wakati ambao unafaa. Mungu hatufunulii mambo yote kwa wakati moja. Katika nyakati hizo ambapo tunasubiri ili Mungu adhihirishe mapenzi yake ndio wakati ambao sisi huweza kukua. "Umngoje BWANA, uwe hodari" (Zaburi 27:14). Wakati mwingi mapenzi yake Mungu huweza kuwa makamilifu maishani mwetu wakati ambao tunamtafuta Mungu na kusubiri miguuni pake. Basi wewe usiwe na wasiwasi, na pia usife moyo katika wakati huo wa kumngoja Mungu. Endelea kuwa mwaminifu na kufanya kila ambacho unajua Mungu anataka ufanye. Mruhusu Mungu kunena nawe kwa njia ambayo Yeye angependa kunena, na kwa wakati ambao Yeye anapenda kufanya hivyo; lakini kamwe usijaribu kwenda mbele kwa hekima yako mwenyewe. Endelea kumtumaini, na uwe na subira nyingi wakati unangoja ili adhihirishe mapenzi yake ya kiungu kwako. Kama hauna uhakika wa mambo basi hebu kuwa na subira.

### 6. Jisalimishe kwa Mapenzi ya Mungu

Hata ingawa Mungu ndiye mtawala mkuu Yeye aliwaumba wanadamu wakiwa na uwezo wa kuchagua mambo watakayofanya, uwezo wa kuamua. Ndiposa ni kweli kwamba mapenzi ya mwanadamu yanaweza kuzamisha mapenzi yake Mungu hivi kwamba yasifanyike maishani mwa mtu, hasa ikiwa mtu kama huyo hafanyi uamuzi wa kibinafsi wa kunyenyekea na kufuata mapenzi ya Mungu. Yesu kwa kweli angeulinda mji wa Yerusalemu, na alikuwa na shauku ya kufanya hivyo, lakini wakazi wa jiji hilo hawakumruhusu kufanya hivyo (Mathayo 23:37). Tunahitaji kutafuta mapenzi yake Mungu kwa kufanya bidii ya kusalimisha shauku zetu za kibinafsi, na yale mambo tunayotaka mikononi mwake Bwana. Watu wengi hutafuta baraka za Mungu katika maamuzi yao, lakini bila kumtafuta Mungu ili mapenzi yake ya kiungu yatendeke. Lakini kwa kweli tunahitaji kuomba kama Kristo alivyoomba: "Si mapenzi yangu, bali yako yatendeke" (Luka 22:42). Kama sisi basi hatuko tayari kujisalimisha kwa mapenzi ya Mungu, tunachotafuta ni kipi?

# Kuishi Maisha ya Utiifu



Ni jambo muhimu kwetu kutafuta mapenzi ya Mungu, huku tukiishi kwa utiifu katika kila fani ya maisha yetu. Hatuwezi kamwe kumtarajia Mungu kudhihirisha mapenzi yake katika sehemu moja ya maisha yetu ambayo tunamtaka atuongoze, ilhali hatuwi watiifu kufuata kile ambacho twajua ni mapenzi yake katika sehemu zingine za maisha yetu. Wakati Mungu amedhihirisha mapenzi yake, kuna baraka kuu inayopatikana kwa mtu kufuata ufunuo huo kwa njia ya kuwa mtiifu kwa mapenzi yake Mungu. "Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi" (Isaya 1:19).

Ni jambo ambalo linawezekana na pia la utukufu mkuu mtu kuishi chini ya uongozi na uvuvio wake Mungu. Wakati tukiandaa mioyo yetu na kumtafuta Bwana, tutaweza kujua na kufanya mapenzi yake. Kujua mapenzi yake ni jambo ambalo huchukua muda wa sisi kukua kama Wakristo, basi wewe usife moyo. Unapoendelea kumfuata Bwana utajifunza kutambua sauti yake na utaweza kuishi na kutembea katika uongozi wake. Mungu atakuongoza na kukuonyesha njia katika safari hii yako ya maisha. Bwana apewe sifa! ■

# Maswali na Majibu

## Je, kuna mapenzi ya kiungu kwa kila uamuzi ambao tunahitaji kufanya?

Mungu hujishughulisha na maisha yetu kwa sababu Yeye anatupenda. Yeye ana mapenzi kwa mambo yote ya kiroho, na pia kwa mambo yote maishani mwetu ambayo yataathiri hali nzuri ya maisha yetu. Lakini kuna maamuzi ambayo ni ya mtu kujichagulia kibinafsi, na ambayo Mungu hana mapenzi dhabiti. Je, utapaka nyumba yako rangi nyekundu au ya buluu? Je, utasafiri kwa gari la usafiri wa umma au gari lako la kibinafsi? Je, utakula viazi au mchele katika chakula chako cha jioni? Mungu huturuhusu kufuata matamanio ya mioyo yetu na Yeye huheshimu yale ambayo tunataka katika fani mbali mbali za maisha yetu ambazo si muhimu sana. Watoto wa Mungu wanahitaji kutumia mapenzi yao ya kibinafsi bila hofu huku mapenzi hayo yao yakidhibitiwa na mapenzi ya jumla ya Mungu kwa watu wote. Ikiwa katika maamuzi hayo ya mambo ambayo sio muhimu sana Mungu ataonelea kuna hatari au kizuizi mbele yetu, tunaweza amini kwamba Yeye atakuwa mwaminifu kutuonyesha jambo hilo wakati ambapo tunahitaji uongozi wake.

## Je, mimi nitatofautisha vipi sauti ya Mungu dhidi ya mawazo yangu ya kibinafsi, na pia sauti ya Shetani?

Wakati ukipita mawazo yetu huweza kubadilika na pia mawazo hayo huathiriwa na hisia zetu. Lakini kamwe sauti ya Mungu haibadiliki. "Mna hila nyingi moyoni mwa mtu; lakini shauri la BWANA ndilo litakalosimama" (Mithali 19:21). Tafsiri moja inasema hivi: "Mwanadamu ana mipango mingi akilini mwake." Mawazo yetu ya kibinafsi hutuletea hali ya kuchanganyikiwa, shaka, na hata masumbufu ya kiakili. Lakini sauti ya Mungu hutuletea amani, utulivu, na uhakika wa mambo, na pia sauti hiyo huandamana na mashahidi wale wengine.
1 Wakorintho 14:33 inasema: "Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu." Hata ingawa andiko hili lazungumzia utaratibu wa kufuatwa katika ibada za sifa, kuna ukweli wa ajabu ambao unapatikana hapa, kwamba "Mungu SIO mwanzilishi wa machafuko." Wakati ambapo tumeandamwa na mawazo akilini mwetu yanayotuletea machafuko na maswali mengi, tunahitaji kutambua kwamba Bwana wetu hatushughulikii kwa njia hiyo. Bwana anaposema nasi sauti yake hutuletea majibu, na tunaweza kutambua mapenzi yake kutoka ndani kabisa ya roho zetu.

Daima dawama sauti ya Mungu hulingana na Neno lake, na kamwe Yeye hatuongozi kwa njia ambayo ni kinyume na kanuni kuu za ukweli. Mimi ninakumbuka miaka mingi iliyopita, wakati ambapo nilimsikia mhubiri wa Injili ambaye mwanzoni alikuwa akihubiri kwamba mtu hastahili kuoa mara ya pili. Sasa nikamsikia akiliambia kanisa lake kwamba Mungu alikuwa amenena naye na kumwambia kwamba hakuna haja ya yeye kuishi kama kapera tena, na kwamba yeye sasa angaliweza kuoa kwa mara ya pili. Kwa kweli jambo hilo halikutokana na Mungu, kwa sababu lilikuwa kinyume na Maandiko. Wakati ambapo unahisi kwamba umepata mwongozo ambao uko kinyume na Neno lake Mungu unaweza kujua kwamba jambo hilo halikutokana na Mungu, bali lilitoka akilini mwako au kutoka kwa Ibilisi.

Wakati mwingine kutakuwa na maswali ya kutaka kujua ikiwa sauti hiyo uliyosikia imetokana na Mungu, au ni ya adui yetu. Hebu tumwangalie mtume Petro wakati wanafunzi wa Yesu walijipata katika dhoruba huko ziwani. Wao waliogopa, lakini Yesu aliweza kujitambulisha mbele yao. Ndipo Petro akamjibu, "Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji" (Mathayo 12:48). Yesu akaweza kudhibitisha kwamba ni Yeye, na mtume Petro akaweza kutembea majini. Bwana akinena ushahidi wa yale yanayopatikana kutokana na sauti hiyo yake utadhihirisha ukweli wa kile ambacho amesema. Shetani ni baba wa uongo, na sisi tunaweza kujifunza kuweza kutambua sauti yake ya udanganyifu.

Hata wakati Shetani aliponakili Maandiko kwa Yesu, yeye alitumia maandiko ya mkato ambayo yalitolewa nje ya muktadha wake. Wakati Ibilisi anaposema, ingawa yeye anaweza kuvalisha sauti yake vazi la kidini, yeye husema mambo ambayo ni ya kimwili, badala ya kusema yale ambayo yanatuleta karibu naye Mungu.

Wakati Mungu amenena nasi kuhusu makosa yetu, hitilafu zetu, au dhambi yetu, Yeye hutupatia suluhisho na njia ya kuweza kurekebisha tatizo hilo. Lakini wakati adui anaposema, yeye hutushtaki na kutusumbua akilini mwetu na pia kutuletea hukumu moyoni mwetu bila kutupatia mweke wa kupata ukombozi. Watu wengi wanaishi chini ya lawama za Shetani, na wao hujihisi vibaya mara nyingi; lakini kwa kweli jambo hilo halitokana na Mungu, kwa sababu hakikisho la kweli la dhambi kutoka kwa Mungu humletea mtu huyo suluhisho, na pia kuandamana na amani moyoni mwake.

JE, WAJUA?

Mungu hulaumiwa kwa sababu ya mambo mengi na watu wa kidini. Watu wengi husingizia "sauti ya Mungu" ili kutoa visingizio kwa maamuzi yao na tabia zao. Lakini ni jambo muhimu sisi tusimtumie Mungu kama kisingizio au kijisababu cha kutaka kufuata njia zetu za kibinafsi, mawazo yetu, au matamanio ya mioyo yetu. Sisi wanadamu tunahitaji kutambua upungufu wetu na upotovu wetu katika swala hili la kumwelewa Bwana na kuelewa mapenzi yake.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# NITAWAONGOZA KWA JICHO LANGU

*Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; nitakushauri, jicho langu likikutazama.*
—Zaburi 32:8



Katika ulimwengu huu ambao umejaa shida na hali ya kuchanganyikiwa, andiko hili ambalo Mungu alimpatia Daudi ni ahadi ya ajabu. Lakini Mungu atatufanyia vivyo hivyo hata katika siku hizi zetu. Katika maswali na mahitaji yetu, Yeye anatuhakikishia kwamba, "Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea." Mungu atatuongoza hata kwenye njia ambazo hatujapitia hapo mbeleni. Yeye atakuwa nahodha wetu na kiongozi wetu, wakati ambapo hatujui njia ya kupitia. Atakuwa mwalimu wetu tunapopitia magumu ya maisha. Atakuwa mshauri wetu katika wakati wetu wa kuchanganyikiwa. Pia atakuwa mchungaji wetu wakati ambapo tumepotea njia. Atakuwa mwanga wetu tunapokuwa gizani, na pia tumaini letu wakati ambapo hatuna uhakika maishani mwetu.

Kwa kweli sisi hatuwezi kujua siku zetu za baadaye zitakuwa vipi, na hatujui kile ambacho tutakumbana nacho kesho. Pia hatujui mitego na hatari ambazo ziko mbele yetu. Lakini Bwana ametwambia kwamba "nitakushauri, jicho langu likikutazama." Yeye ataenda mbele zetu na kufichua hatari zilizoko mbele yetu. Atatutunza kwa makini kuhakikisha kwamba barabara tunayopitia iko na mwangaza. Na wakati tukipatwa na vizuizi safarini Mungu atatuinua juu au kutuonyesha njia ya kuepuka vizuizi hivyo. Na wakati tukianguka, Yeye atatuona na kutunyoshea mkono wake na kutuinua. Ikiwa katika uanadamu wetu tutapotea njia, Yeye atakuja kututafuta na kutuongoza kurudi katika kundi lake.

Sisi ni watu dhaifu na ambao hatuna utoshelevu wa maisha, na kwa kweli sisi hatujui maamuzi bora katika maisha yetu kwa mambo mengi tunayokumbana nayo. Lakini Bwana ameahidi kwamba atatuongoza na kutusaidia. Yeye atatuonyesha njia na kutuletea uwezo wa kuelewa mambo katika hali hiyo ya kuchanganyikiwa kwetu. Jicho lake linatutazama. Mtoto wa Mungu hana haja ya kusumbuka au kuogopa. Ni jambo ambalo mimi linaniletea faraja na usalamu kujua kwamba Bwana wangu mwenyewe ananitunza.

"Tazama, jicho la BWANA li kwao wamchao, wazingojeao fadhili zake" (Zaburi 33:18). Mungu anawajali watu wote, lakini Yeye huwa makini sana kwa wale ambao wanamheshimu na kumwamini.

Kama vile Mungu humwona shomoro ambaye ameanguka chini, jicho lako linakutazama wewe. Basi jipe moyo wewe askari mwenzangu. Mungu atakuongoza na kukufikisha upande ule mwingine ukiwa salama salimini. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana